Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Omari Kigua, akiuliza swali bungeni Dodoma jana kuhusu lini serikali itajenga kituo cha polisi katika Wilaya ya Kilindi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

NIPASHE UK 8.

# Mbunge: Hali ya upatikanaji samaki Ziwa Victoria mbaya

MBUNGE wa Muleba Kusini (CCM), Dk. Oscar Kikoyo, amesema hali ya Ziwa Victoria hususan upatikanaji wa mazao ya samaki ni mbaya huku samaki wazazi wakiwa chini ya asilimia 0.85.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, mbunge huyo alisema kulingana na viwango takiwa, kwenye ziwa lolote samaki wazazi wanapaswa kuwa kati ya asilimia tatu hadi tano lakini kwa takwimu zilizotolewa na serikali kwenye ziwa hilo, samaki wazazi wapo chini ya asilimia 0.85.

"Upungufu huo hauhusiani na uvuvi haramu? Task forces (vikosi kazi) zipo Ziwa Victoria, hawa wanaotumwa kwenda kufanya kazi ni wasomi lakini hawana weledi wowote na masuala ya uvuvi na matokeo yake wamekuwa wakikamata hizo zana haramu wanawapiga faini zisizo na kanuni wala sheria, baada ya kuwapiga faini wanawarudishia zana haramu, sasa serikali haioni inaendekeza uvuvi haramu?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema upungufu wa samaki wazazi unahusiana na uvuvi haramu.

"Tumeweka mkakati shirikishi kupitia vyombo vyetu ambao utakwenda kunusuru hali ile kwanza kulinda samaki wazazi na rasilimali nzima, ili kuwa na uendelevu wa rasilimali hii muhimu kwa nchi yetu," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema inawezekana kuna maofisa wanaofanya kazi kinyume cha maelekezo ya serikali na watachukua hatua madhubuti kwa wale wanaoharibu operesheni za kulinda rasilimali za nchi.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni kwa kiwango gani vikosi kazi vimepunguza tatizo la uvuvi haramu kwenye Ziwa Victoria kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.


Ulega, akijibu swali hilo, alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/2018 hadi 2019/2020, Kikosi Kazi kilifanya doria na operesheni kwenye maeneo mbalimbali ya ukanda wa Ziwa Victoria.

"Utekelezaji wa doria hizo uliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika shughuli za uvuvi ikiwamo nyavu za makila, makokoro, nyavu za timba (Monofilament) na nyavu za dagaa.

"Pia, vifaa vilivyokuwa vinatumika kwenye uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi ikiwamo injini za boti pamoja na gari," alisema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa doria hizo kwenye maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria uliwezesha kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi kwa asilimia 80.

CamScanner



*HABARI LEO UK 7.*





# Uvuvi haramu waathiri samaki kuzaliana

SHUGHULI za uvuvi haramu zinazoendeshwa na watu wasiokuwa waaminifu zimechangia kwa kiasi kikubwa upungufu wa samaki mama katika Ziwa Victoria.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega (pichani) alisema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Muleba Kusini, Dk Oscar Kikoyo aliyetaka kufahamu endapo upungufu wa samaki mama hauhusiani na uvuvi haramu.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, serikali kupitia vyombo vyake vyote inatekeleza mkakati utakaonusuru na kulinda samaki wazazi pamoja na rasilimali nzima ya samaki katika ziwa hilo.

"Yawezekana wako maofisa wanaofanya vitendo vilivyo kinyume na maelekezo na maagizo ya serikali. Serikali ipo tayari kuwachukulia hatua madhubuti yeyote anayethubutu kuhujumu mipango ya serikali," aliongeza Ulega.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/2018 - 2019/2020, kikosi kazi kilifanya doria na oparesheni katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na kuwezesha kukamatwa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika shughuli za uvuvi ikiwamo nyavu za makila, makokoro, nyavu za timba na nyavu za dagaa.

Alisema utekelezaji wa doria hizo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria uliwezesha kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi kwa asilimia 80.

"Wote tunahitaji mchakato wa Katiba ukamilike ili tupate Katiba

kana kama kuna utashi wa kisiasa, yale yote yanayoleta utata ndani

mdau wa siasa.

majukwaa haya ilikuwa ni kuwawezesha viongozi wa vyama vya siasa kati-

sauti za wananchi zinasikika kupitia majukwaa ya siasa.

MWANANCHI UK5.

# 'Marufuku wa nje kununua mifugo kwa wakulima'

**Aurea Simtowe na Sharon Sauwa,**
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar/Dodoma.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amepiga marufuku wanunuzi kutoka nje nje ya nchi kwenda vijijini badala yake wanunue mifugo kwenye minada ya upili na mipakani.

Ili kukomesha vitendo hivyo, amesema hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa Watanzania watakaobainika kuwasaidia wageni hao kununua mifugo nje ya minada.

Wakati Waziri Ndaki akipiga marufuku hiyo, Bunge limeitaka Serikali kuweka mazingira yatakayowezesha kusafirisha nyama nje ya nchi na kuachana na utaratibu wa kuuza mifugo ili kuongeza mapato na ajira nchini.

Waziri Ndaki alitoa kauli hiyo alipojibu malalamiko ya wafanyabiashara wa ng'ombe katika Mnada wa Pugu jijini Dar es Salaam ambao walisema wageni kuruhusiwa kununua mifugo kutoka kwa wafugaji kumepaisha bei ya ng'ombe kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuliko upatikanaji.

Akizungumza katika hafla ya kupokea mizani 82 itakayofungwa katika minada mbalimbali nchini, Nestory Lukaya, mfanyabiashara wa mnadani hapo alisema wafanyabiashara kutoka nje wamesababisha mfumuko wa bei.

"Wao wananunua ng'ombe kule mnadani halafu sisi hapa hatupati, tunabaki na mifumuko ambayo haina tija. Kwa ujumla, hata nyama inapanda bei na wananchi wanashindwa kupata kitoweo kwa bei rafiki," alisema Lukaya.

Akijibu suala hilo, Waziri Ndaki alisema wanunuzi kutoka nje wanatakiwa kununua mifugo husika katika minada ya upili.

"Hairuhusiwi kwa mgeni kununua mzigo moja kwa moja kwa wafugaji, haruhusiwi kwenda yeye kununua mnadani (minada ya awali), ipo minada yetu ya upili hiyo ndiyo inatoa kibali cha kusafirisha mifugo kwenda nje. Ipo minada ya mipakani na yenyewe inatoa kibali mifugo kusafirishwa lakini kinachofanyika ni mfanyabiashara wa Tanzania anajifanya mwenyeji wa huyo mgeni ananunua mifugo kwa jina lake halafu anamsaidia na namna ya kuitorosha," alisema.



Ng'ombe akipimwa uzito kwenye mzani maalumu wakati wa uzinduzi wa uliofanyika katika Mnada wa Pugu mkoani Dar es Salaam jana. **Picha na Michael Matemanga**

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mifugo na Mazao yake Vingunguti, Joel Meshack alisema Mkoa wa Dar es Salaam unachinja mifugo mingi lakini ndio unaoongoza kwa kufanya biashara kinyume na utaratibu.

"Mtu anao uwezo wa kununua ng'ombe bila kuulizwa anapeleka wapi na akifika machinjioni haulizwi jambo ambalo limefanya kuuzwa holela mitaani," alisema.

Akijibu hoja hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Amani Mafuru alisema wako mbioni kutoa vitambulisho kwa wachinjaji ambavyo vitazuia uuzaji holela wa nyama hasa ambayo haijathibitishwa kwa matumizi.

**Ushauri wa Bunge**

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kamati hiyo jana kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023, aligusia usafirishaji nyama.

Alisema kamati ilipokea taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu mikakati ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

"Usafirishaji wa mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo unahesabiwa kama sehemu ya mafanikio ilhali unaathiri ajira na kupunguza thamani ya mauzo nje.Hadi Oktoba 2022 takriban ng'ombe, mbuzi na kondoo 4,000 walisafirishwa kwenda Bara la Asia na kuhesabiwa kuwa mafanikio," alisema.

), Salim zaidi ya ɔia kupi-

za wazee, hivyo kama madirisha yao hayana huduma watafuatilia na kuwajibisha wahusika.

MWANANCHI UK 20.

# Wanawake wajitosa uvuvi wa samaki

**Burhani Yakub, Mwananchi**
**byakub@mwananchi.co.tz**

**Tanga.** Wanawake wa Pwani ya Bahari ya Hindi katika Kijiji cha Tongoni Wilaya ya Tanga wameushangaza umma baada ya kuamua kujitosa kwenye shughuli za uvuvi na kuibuka kundi linalotegemewa kwa shughuli ambayo awali ilikuwa ya wanaume.

Kumekuwa na hulka na dhana katika jamii kuwa wanawake hawawezi kuendesha shughuli za uvuvi, lakini hali ni tofauti baada ya wanawake kuunda vikundi viwili vya uvuvi katika Bahari ya Hindi.

Kutokana na juhudi hizo, wanawake hao walionwa na wafadhili kutoka shirika la kimataifa la Botna, likawapatia boti mbili za kisasa na kuwa miongoni mwa vikundi 12 vya wavuvi vilivyopewa boti hizo mkoani Tanga.

Mwenyekiti wa Kikundi cha wanawake wavuvi Tongoni, Hadija Abdallah alisema hawaogopi maji ya bahari kwa sababu wamezaliwa katika pwani hiyo, hivyo tangu wakiwa wadogo shughuli zao nyingi zinategemea bahari.

**"Hapa kwetu hakuna mwanamke ambaye haingii baharini, tunaweza kuogelea, kuendesha vyombo vya majini na hata kuvua, kwa hivyo si jambo geni na wameweza kujikwamua kiuchumi."**
Hadija Abdallah

Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Neema John alisema vikundi hivyo viwili vya wanawake kati ya 12 vikiwamo vya vijana vilivyokabidhiwa boti vimeshaweka akiba ya Sh2 milioni, tofauti na wenzao kutokana na na mafunzo ya ujasiramali waliyopewa.

Mbali na boti, vikundi hivyo vilipewa majaketi ya kujiokoa, visanduku vya huduma ya kwanza na vifaa vingine vya uokozi.



ısajili ı ajali na.

ŋjaro, bu ni ɔ hai- i kwa yake. ‹A na rafiki anchi

una- o kis- ku za ı hizo ea na

i wa l Ben- a utii lia tu